## Maswali

1. Taifa la Israeli lilimpenda na kutii Mungu?
2. Taifa gani kubwa lilishambulia Israeli?
3. Watu wa Israeli waliamini Mungu?
4. Nini ilifanyika kwa watu wa Israeli?
5. Mfalme wa Ashuru alitumia Hezekia ujumbe gani?
6. Hezekia alifanya nini?
7. Mfalme alituma nini kwa Hezekia?
8. Hezekia alifanyaje hiyo barua?
9. Ujumbe gani Mungu alimtumia Hezekai?
10. Nini ilifanyika kwa Waashuru?

## Majibu

1. Hapana, watu wa Israeli waliabudu sanamu.
2. Taifa la Ashuru lilishambulia Israeli.
3. Hapana.
4. Walichukuliwa mateka mpaka Ashuru.
5. Usiamini Mungu. Hatakuokoa kutoka kwa Waashuru.
6. Hezekia aliomba Mungu, na alituma wamuite nabii Isaya.
7. Alituma barua kwa Hezekia akisema Mungu hatamuokoa.
8. Hezekia alipeleka barua kwa nyumba ya Mungu na akaomba.
9. “Usiogope, Waashuru hawatashambulia Yerusalemu.”
10. Ugonjwa uliuwa Waashuri 185,000. Wengine walienda kwao na mfalme wao alikufa

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1    Mwaka wa 2**

# 26 Mfalme Hezekia

## Marejeo

2 Wafalme 18:28—30 na 35—37

2 Wafalme 19:1—16 na 32—37

## Kiini cha somo


Kuonyesha kwamba Mungu ako karibu na wampendao. Hakuna kisichowezekana tukiwa na imani kwa Mungu.

## Maneno maalum

1. Kiasi + sanamu + miaka 200 + hawakutubu.
2. Ashuru + Samaria + zingirwa + miaka 3 + hakuna chakula.
3. Hezekia + ujumbe + lisha watu.
4. Omba + Isaya + Mungu atasaidia + usiogope.
5. Barua + Mungu hawezi kuokoa + omba.
6. Mungu akasikia maombi + Waashuru wauwawa.
7. Hakuna kisicho wezekana kwa Mungu.

**26.1** Kwa mda mrefu watu wa ufalme wa Israeli waliasi amri za Mungu. Waliabudu sanamu za miti na mawe. Hawakumpenda Mungu. Mungu alipenda taifa la Israeli na alitaka wamrudie. Mungu aliongoja kwa miaka 200 watubu na wamrudie lakini hawakutubu. Bado waliabudu sanamu.

**26.2** Ashuru lilikuwa taifa kubwa. Waashuru walipigana na watu wa Israeli. Mfalme wa Ashuru aliwashurutisha Waisraeli watoe pesa ya kodi kila mwaka. Mwaka fulani watu wa Israeli waliasi. Walikataa kulipa kodi ya pesa kwa mfalme wa Ashuru, alikasirika sana. Akaleta jeshi lake kupigana na Israeli. Waashuru walizingira Samaria mji mkuu wa Israeli. Mfalme wa Ashuru pamoja na jeshi lake walipiga kambi Samaria. Hakuna aliyetoka wala kuingia mjini, waliwazingira kwa miaka mitatu. Baada ya hiyo miaka mitatu watu wa Israeli hawakukuwa na chakula. Wakajisalamisha kwa Waashuru. Mfalme wa Ashuru aliwachukuwa watu wa Israeli wote na kuwapeleka Ashuru wawe mateka na watumwa wao .Aliendelea kuwa na nguvu na kushinda falme zingine nyingi. Aliwachukuwa mateka watu wengi.



**26.3** Mwaka mmoja, Hezekia mfalme wa Yuda alikataa kulipa kodi kwa mfalme wa Ashuru. Waashuru walienda kushambulia Yuda. Waashuru waliharibu vijiji vingi tena waliendelea ili washambulia Yerusalemu mji mkuu wa Yuda. Mfalme wa Ashuru alituma wajumbe Yerusalemu kwa mfalme Hezekia. Wajumbe walipeana ujumbe kwa watu wote wa Yerusalemu kwa sauti. Watu wa Yerusalemu walikusanyika kwa ukuta wa Yerusalemu kusikiliza maneno kutoka kwa Ashuru. Waashuru walitisha watu wote. Walitoa sauti na kusema, “Musimsikilize Hezekia, hatawaokoa kutoka kwa Waashuru. Hezekia atawambia kuamini Mungu. Msimsikilize, Mungu wenu hawezi kumuokoa kutoka kwa jeshi la Ashuru lenye nguvu. Tumeshinda nchi nyingi. Mungu wa hao watu hakuwaokoa. Mungu wenu hatawaokoa kutoka kwa Waashuru, jisalamishe kwa mfalme wa Ashuru.”

**26.4** Watu wa Yerusalemu walikuwa wamekatazwa kujibu wale wajumbe. Walisikiliza hali wako kimya. Mfalme Hezekia alisikia ujumbe, alirarua nguo zake na kuweka jivu kwa kichwa chake kuonyesha huzuni. Hezekia aliomba Mungu, aliuliza Mungu awasaidie. Akatuma wamuite nabii Isaya, Isaya akamletea habari kutoka kwa Mungu. Mungu alisema hivi, “Usiogope Waashuru, nitawarudisha kwa nchi yao. Mfalme wa Ashuru atarudi kwa nchi yake na akufie huko.”

**26.5** Mfalme wa Ashuru akatumia Hezekia barua, akisema, “Mungu wako hawezi kukuokoa. Mungu wako hatazuia Waashuru kuchukuwa Yerusalemu. Tumeshinda na kuharibu nchi nyingi, tutakuja tuharibu Yerusalemu na Yuda. Hakuna miungu ya watu wengine wanaookoa. Mungu wako hatakuokoa.” Hezekia alichukua barua na kupeleka kwa nyumba ya Mungu, akaomba Mungu, “Ee Bwana Mungu, wewe ni Mungu wa falme zote duniani, wewe ni Mungu waajabu aliyeumba mbingu na nchi. Tafadhali tuokoe kutoka kwa Waashuru. Tafadhali onyesha nguvu zako ili mataifa yote yajue wewe ndiwe Bwana Mungu. Wewe ndiye Mungu pekee.” Hezekia aliamini Mungu na Mungu akawaokoa kutoka kwa Waashuru. Isaya alimletea Hezekia habari ingine kutoka kwa Mungu. Mungu alimwambia Hezekia, “Mfalme wa Ashuru hatakuja hapa jijini, hatapiga mshale hapa, atarudi kwa nchi yake.”

**26.6** Jeshi la Ashuru lilienda kushambulia Yerusalemu na wakaenda mpaka karibu na kijiji cha Nobu. Usiku huo, Mungu alituma ugonjwa uliouwa watu 185,000 wa jeshi la Ashuru. Waashuru waliogopa sana, asubuhi mapema Waashuru walitoroka na kurudi kwao. Mfalme wa Ashuru aliuwawa na wana wake wawili huko nyumbani.

**26.7** Somo hili linatufunza kwamba Mungu ako karibu na wanaompenda. Hakuna lisilowezekana kwa Mungu. Hakuna nguvu inayomshinda. Taifa la Israeli halikumsikiza Mungu, walichukuliwa mateka na Waashuru. Hezekia na taifa la Yuda walimuamini Mungu. Mungu aliwaokoa kutoka kwa jeshi la nguvu la Ashuru.